



TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 26 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

TAARIFA INATOLEWA KWAMBA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA SITA (26) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB UTAFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE (JNICC), DAR ES SALAAM SIKU YA JUMATANO TAREHE 10 JUNI, 2026 KUANZIA SAA 4 ASUBUHI.

AJENDA YA MKUTANO ITAKUWA KAMA IFUATAVYO:

- 26.1 TAARIFA NA AKIDI
- 26.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 26.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 25 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2025
- 26.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 25 WA WANAHISA
- 26.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2025
- 26.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2025
- 26.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA VIWANGO VYA MALIPO YA WAKURUGENZI
- 26.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
- 26.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2026
- 26.10 KUIDHINISHA UANZISHWAJI WA MAKAMPUNI TANZU
- 26.11 KUIDHINISHA MAPENDEKEZO YA MABADILIKO YA MUUNDO
- 26.12 MENGINEYO

MAELEZO MUHIMU

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano anatakiwa kuwasilisha namba ya CDS, kama inavyoonekana katika Hati ya Uwekezaji wa Hisa (Depository Receipt) pamoja na kitambulisho halali.
2. Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata / kuzingatia Sheria na Katiba za Kampuni. Fomu ya uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Benki (www.nmbbank.co.tz) na kwenye matawi ya Benki ya NMB. Fomu ya uwakilishi iwasilishwe kwenye ofisi ya Katibu wa Kampuni, NMB Makao Makuu au kwa njia ya kielektroniki kwa barua pepe Farija.Ghikas@nmbbank.co.tz kabla ya Saa 4 asubuhi Jumanne tarehe 9 Juni 2026.
3. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake.
4. Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza malipo gawio la kawaida la TZS 504.26 kwa kila hisa, pamoja na gawio maalum la TZS 105.89 kwa kila hisa, hivyo kufanya jumla ya gawio lililopendekewa kuwa TZS 610.15 kwa kila hisa. Hii inawakilisha jumla ya malipo ya gawio ya TZS 305.08 bilioni kutoka kwenye faida baada ya kodi ya mwaka 2025 ya TZS 756 bilioni.

TAREHE ZA KUZINGATIA

- Tarehe ya Tangazo: - 20 Mei 2026
- Hisa kuuzwa pamoja na gawio: - 20 Mei 2026
- Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio: - 10 Juni 2026
- Hisa kuanza kuuzwa bila gawio: - 11 Juni 2026
- Daftari la wanahisa kufungwa: - 12 Juni 2026
- Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe: - 24 Juni 2026

Kwa Amri ya Bodi.



Farija Ghikas
Katibu wa Kampuni
20 Mei 2026